**HOTUBA YA BIBI. BENG'I M. ISSA, KATIBU MTENDAJI WA BARAZA LA TAIFA LA UWEZESHAJI WANANCHI KIUCHUMI KATIKA KONGAMANO LA TAIFA LA SITA LA UWEZESHAJI WANANCHI KIUCHUMI LILILOFANYIKA TAREHE 19 SEPTEMBA, 2022, KATIKA UKUMBI WA PSSSF, DODOMA**

Mhe. Kassim M. Majaliwa, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania

Mhe. Dkt. Ashatu Kijaji, Waziri wa Uwekezaji, Viwanda na Biashara

Waheshimiwa Mawaziri;

Mhe. Exuad Kigahe, Naibu Waziri, Uwekezaji, Viwanda na Biashara;

Waheshimiwa Manaibu Waziri;

Mhe. Rosemary Senyamule, Mkuu wa Mkoa wa Dodoma;

Waheshimiwa Wakuu wa Mikoa;

Makatibu Wakuu wa Wizara,

Bw. Ally Gugu, Kaimu Katibu Mkuu, Uwekezaji;

Makatibu Tawala wa Mikoa,

Waheshimiwa Wakuu wa Wilaya za Dodoma,

Wakurugenzi wa Halmashauri,

Prof. Aurelia Kamuzora, Mwenyekiti wa Baraza la Taifa la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi;

Wajumbe wa Baraza la Taifa la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi;

Wakuu wa Taasisi za Serikali,

Wadau wa Maendeleo;

Wakuu wa Taasisi za Sekta Binafsi na Asasi za Kiraia;

Waandaaji Wenza wa Kongamano (Taasisi ya Uongozi na REPOA)

Wadhamini wa Kongamano;

Wawakilishi kutoka Taasisi za Serikali na Sekta Binafsi;

Waratibu wa Uwezeshaji wa Wizara, Taasisi, Mikoa na Halmashauri mbalimbali;

Wanahabari;

Wageni Waalikwa;

Mabibi na Mabwana

**Nawasalimu kwa Jina la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania**

**Mheshimiwa Mgeni Rasmi**

Awali ya yote ninapenda kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa Rehma kwa kutuwezesha wote kushiriki katika Kongamano hili la Sita la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi. Natoa shukrani zangu za dhati kwako Mhe. Waziri Mkuu wa Jamhuri wa Muungano wa Tanzania, kwa kukubali kuwa mgeni rasmi katika Kongamano hili na kutenga muda kuja kuiheshimisha shughuli hii. Aidha, niwashukuru washiriki wote kutoka ndani na nje ya jiji la Dodoma kwa ushiriki wenu pamoja na majukumu makubwa na ya muhimu mliyonayo. Hii inadhihirisha dhamira njema mliyo nayo

katika kuhakikisha watanzania wanawezeshwa kushiriki kikamilifu katika uchumi wa nchi.

**Mheshimiwa Mgeni Rasmi**

Kongamano hili linahudhuriwa na jumla ya washiriki 500. Naomba nichukue fursa hii kuwatambulisha waliohudhuria katika kongamano hili ambao bado hawajatambulishwa:

- Wajumbe wa Baraza la Taifa la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi
- Wajumbe wa Kamati ya Kitaifa Ushauri wa Utekelezaji wa Ahadi za Nchi katika Kizazi chenye Usawa wa Kijinsia (Generation Equality Forum)
- Wadhamini wa Kongamano
- Wakuu wa Taasisi wa Serikali
- Wakuu wa Taasisi za sekta binafsi,
- Wadau kutoka Asasi za Kiraia,
- Viongozi wa Taasisi mwavuli za vikundi vya kifedha vya kijamii,
- Viongozi na wataalam kutoka Taasisi za Elimu na utafiti
- Viongozi na wawakilishi kutoka Mifuko ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi
- Vyombo vya habari
- Waratibu wa uwezeshaji kutoka Mikoani na wilayani
- Waratibu wa Local Content
- Wafanyabiashara, Wawekezaji na Wajasiriamali
- Wafanyakazi wa Baraza la Taifa la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi
- Wageni wengine wote maalum walioalikwa.

**Mheshimiwa Mgeni Rasmi**

Baraza la Taifa la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi lina jukumu la kusimamia, kufuatilia na kuratibu shughuli za uwezeshaji kama ilivyoainishwa katika Sera na Sheria ya Taifa ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi ya mwaka 2004. Aidha, Sera ya Taifa ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi ina lengo la kuhakikisha kwamba watanzania wanapata fursa ya kushiriki kikamilifu katika uchumi wa nchi, ili kutekeleza Dira ya Maendeleo ya Taifa ya mwaka 2025.

Shughuli za uwezeshaji wananchi kiuchumi zimekuwa zikifanyika katika sekta zote hapa nchini, kuanzia ndani ya Serikali mpaka nje ya Serikali. Hapa nina maana Wizara, Mikoa, Halmashauri, Taasisi za Serikali, Kampuni Binafsi, Asasi za KIraia na wajasiriamali. Ni wajibu wa Baraza kufuatilia na kutathmini utekelezaji unaofanywa na wadau wote hawa hapa nchini.

Baraza limekuwa likifanya Kongamano la Uwezeshaji wa Wananchi Kiuchumi mara moja kwa mwaka tangu mwaka wa fedha 2015/2016 ikiwa ni sehemu ya utekelezaji wa Mkakati wa Utekelezaji wa Mwongozo wa Taifa wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi.

**Mheshimiwa Mgeni Rasmi**

Kongamano hili la Sita la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi linakutanisha wadau mbalimbali wakiwemo viongozi wa Serikali, Sekta binafsi, Taasisi za elimu na utafiti, Wadau wa Maendeleo na Asasi za Kiraia. Lengo la Kongamano hili pamoja na mambo mengine ni:

1. Kuongeza ufahamu wa wadau mbalimbali kuhusu dhana ya uwezeshaji kiuchumi na kuwafahamisha majukumu waliyo nayo katika kuwawezesha watanzania;

2. Kupeana uzoefu katika kutekeleza shughuli za uwezeshaji wananchi kiuchumi;
3. Kuzindua Taarifa ya mwaka ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi;
4. Kutambua mchango na jitihada zilizofanywa na wadau mbalimbali wakiwemo Wizara, Taasisi za Serikali, Taasisi binafsi, Taasisi za elimu, Mikoa, Wajasiriamali katika kutekeleza shughuli za uwezeshaji wa wananchi kiuchumi kwa kuwatambua na kuwapa tuzo;

**Mheshimiwa Mgeni Rasmi,**

Kauli Mbiu ya Kongamano la mwaka huu ni **UWEZESHAJI WANANCHI KATIKA UWEKEZAJI.** Kauli mbiu hii inalenga kutambua jitihada za Serikali ya awamu ya sita ambayo inalenga kuimarisha sekta binafsi na kuhakikisha kunakuwa na mazingira bora kwa watanzania kuwekeza na kunufaika na uwekezaji unaofanyika hapa nchini. Aidha, inalenga pia kuhamasisha wadau mbalimbali kuunga mkono jitihada za Serikali za kuwawezesha watanzania kushiriki katika uwekezaji.

**Mheshimiwa Mgeni Rasmi,**

Tangu asubuhi tulipofika hapa tumekuwa na majadiliano ya kuangalia utekelezaji wa Sera ya Uwezesahji Wananchi Kiuchumi katika mikoa ya ……………………., …………………….., ………………………….. na ……………………………………. Ambapo waheshimiwa wakuu wa mikoa husika wameshiriki katika majadiliano.

Vilevile kulikuwa majadiliano ya wataalam kutoka EACOP (Msimamizi wa mradi wa Bomba la Mafuta Ghafi kutoka Hoima -

Uganda mpaka Chongoleani - Tanga) kujadili ushiriki wa watanzania katika mradi huo, TAWLA (Taasisi ya Wanasheria Wanawake) kujadili haki za wanawake na uwezeshaji wa wanawake kiuchumi, REPOA (Taasisi ya utafiti) masuala muhimu yanayotokana na tafiti kwa ajili ya kuboresha uchumi na hali ya watanzania kiuchumi na Taasisi ya Uongozi kwa ajili ya kuboresha ushiriki wa wanawake kwenye uongozi na uchumi.

**Mheshimiwa Mgeni Rasmi**

Mnamo mwaka 2018 uliekeza Baraza kusimamia na kuratibu uanzishwaji wa vituo vya uwezeshaji wananchi kiuchumi nchi nzima napenda kutoa taarifa kuwa mpaka sasa hivi kuna vituo 18 katika mikoa ifuatayo: Dodoma, Singida, Shinyanga, Geita, Rukwa na Kigoma. Vituo hivi kwa mwaka wa fedha 2021/2022 vimeweza kuhudumia jumla wa watanzania 11,799 ambao wanawake walikuwa 6,157 (52%) na wanaume 5,642 (48%) na jumla ya mikopo ya shilingi bilioni 28 imetolewa katika vituo hivyo ikiwa ni ongezeko la 14% kutoka kwenye mikopo iliyotolewa kwa mwaka 2020/2021 na jumla ya biashara 15,860 zimeweza kurasimishwa katika vituo hivi.

Vilevile, katika hatua za kuongeza vituo hapa nchini Baraza limekamilisha mapitio ya mwogozo wa kuanzisha na kusimamia vituo hivi ambao unatambua uwepo wa vituo vingine vya huduma mahali pamoja yaani (One Stop Centres) ambazo zipo mikoani ili kuongeza huduma za uwezeshaji katika vituo hivyo. Katika suala hili Baraza linaendelea na utaratibu wa kuunganisha jitihada za mpango wa MKURABITA wa kutambua vituo vyao na kuongeza huduma za uwezeshaji na pia Mikoa ya Morogoro na Pwani iko kwenye hatua za mwisho za kuongeza huduma za uwezeshaji

katika vituo vyao vya kutoa huduma kwa pamoja ili viweze kutumika kama vituo vya uwezeshaji. Baraza limekubaliana na waratibu wa ngazi za mikoa na halmashauri kuongeza juhudi za uanzishaji wa vituo hivi.

**Mheshimiwa Mgeni Rasmi**

Serikali imeendelea kutekeleza miradi ya kimkakati na kuongeza uwekezaji hapa nhini. Jukumu kubwa la Baraza ni kusimamia ushiriki wa watanzania katika miradi hiyo na uwekezaji unaofanyika hapa nchini. Miradi ya Kimkakati iliyoendelea kutelekezwa nchini na Serikali ni pamoja na Mradi wa ujenzi wa bwawa la kufua umeme la Julius Nyerere (JNHPP), Mradi wa Ujenzi wa Reli ya Kisasa (SGR), Mradi wa Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki (EACOP), Ujenzi wa Barabara na madaraja marefu, Miradi ya maji, Uwekezaji katika migodi (Madini), Nishati, Mafuta na Gesi Asilia. Utekelezaji wa ushiriki wa watanzania katika miradi ya kimkakati na uwekezaji katika kipindi cha mwaka 2021/2022 kwenye ajira ni watu 83,254 wamepata ajira za moja kwa moja na ajira zisizo za moja kwa moja ni watu 361,975. Aidha, Manunuzi ya bidhaa za kampuni za kitanzania na watoa huduma wa kitanzania imezingatiwa katika uendeshaji wa miradi ya kimkakati na uwekezaji nchini. Katika mwaka 2021/2022 jumla ya kampuni 1771 za kitanzania zimepata kazi na kuuza bidhaa kwenye miradi na uwekezaji hapa nchini. Katika Mafunzo na uhaulishaji wa teknolojia kwa wazawa ili kujenga uwezo wa watanzania waliopata ajira katika miradi hiyo Serikali imeweka utaratibu maalum wa kujenga uwezo wa watanzania katika uendeshaji na utengenezaji wa reli ya SGR mara itakapoanza kufanya kazi. Vilevile watanzania wameandaliwa kuendesha mitambo na kufanya matengenezo mara baada ya Bwawa la

Kufua Umeme la Mwalimu Nyerere litakapowakamilika.

**Mheshimiwa Mgeni Rasmi**

Baraza limeendelea kuratibu na kusimamia mifuko ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi hapa nchini. Sasa hivi kuna jumla ya Mifuko na programu za uwezeshaji wananchi kiuchumi 85 ambazo zinaratibiwa na Baraza la Uwezeshaji na ambazo imegawanyika katika makundi makuu manne ambayo ni Mifuko inayotoa mikopo moja kwa moja kwa walengwa, Mifuko inayotoa dhamana kwa kushirikiana na Taasisi za fedha, Mifuko inayotoa ruzuku na Programu za Uwezeshaji. Kati ya mifuko na programu hizo, mifuko na programu 75 zinamilikiwa na Serikali na mifuko/ programu 10 zinamilikiwa na Sekta binafsi. Aidha, Mifuko inayotoa mikopo moja kwa moja ipo 24 (28%), mifuko inayotoa dhamana ipo 13 (15%), mifuko inayotoa ruzuku ipo 32 (38%) na Programu za uwezeshaji zipo 16 (19%). Mifuko ya uwezeshaji inayotoa mikopo moja kwa moja kwa kushirikiana na ile inayotoa dhamana imefanikiwa kutoa mikopo yenye thamani ya shilingi Trilioni 5.68 kwa wajasiriamali 9,435,455 ambapo miongoni mwao wanawake ni 4,959,890 ambao sawa na asilimia 52.7 na wanaume 4,475,566 sawa na asilimia 47.3. Aidha, miongoni mwa mikopo yote iliyotolewa, kiasi cha shilingi bilioni 5.51 zilitolewa kwa watu wenye ulemavu 717,095. Aidha, tathmini inaonyesha kuwa sekta zilizonufaika kupitia mifuko ya uwezeshaji na programu zake kwa kiwango kikubwa ukilinganisha na Sekta zingine ni Kilimo na Ufugaji (23.4%) huku ikifuatiwa na Sekta ya Viwanda na Biashara (20.9%).

**Mheshimiwa Mgeni Rasmi**

Baraza limeendelea kufuatilia utekelezaji wa shughuli za majukwaa ya uwezeshaji wanawake kiuchumi ambayo yalianzishwa mwaka 2017. Hadi sasa kuna jumla ya majukwaa 3,091 ambayo yameanzishwa kwenye Mikoa yote 26 ya Tanzania Bara, Halmashauri 140, Kata 1,149, Mitaa/Vijiji 1,776. Majukwaa haya yamesajiliwa kama vikundi na mpaka sasa kuna jumla ya vikundi 3,430 ambavyo vimesajiliwa kama majukwaa. Vilevile majukwaa yametoa mafunzo kwa wanawake na jumla ya wanawake 42,300 wamepata mafunzo kwenye masuala ya uongozi, ujasiriamali, urasimishaji biashara, nidhamu ya fedha, mikopo n.k.

**Mheshimiwa Mgeni Rasmi**

Siku ya leo ni siku adhimu sana kwetu sisi kwa sababu hufanyika mara moja tu mwaka. Katika mambo ambayo utayafanya siku ya leo ni pamoja na:

i. Kuzindua taarifa ya utekelezaji wa Sera ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi ya mwaka 2021/2022, ambayo imeeleza utekelezaji wa Sera ya Uwezeshaji katika sekta mbalimbali hapa nchini na hatua ambazo tumezipiga katika utekelezaji.
ii. Leo hapa vilevile Mhe. Waziri Mkuu utatoa tuzo kwa Wizara zilizofanya vizuri katika shughuli za uwezeshaji wa watanzania, Mikoa iliyofanya vizuri kwenye shughuli za uwezeshaji, Taasisi zilizo fanya vizuri, mifuko ya uwezeshaji iliyofanya vizuri, makampuni binafsi yaliyofanya vizuri, Vyuo vikuu vilivyofanya vizuri, wajasiriamali na Asasi za kiraia zilizofanya vizuri.

**Mheshimiwa Mgeni Rasmi**

Mwisho kabisa ila sio kwa umuhimu napenda kutoa shukrani za dhati kwa Taasisi za REPOA na UONGOZI kwa kushirikiana nasi kuandaa kongamano hili. Pia napenda kuwashukuru sana wadhamini wote waliojitoa kwa hali na mali kufanikisha Kongamano hili ambao ni Mdhamini Mkuu Benki ya STANBIC na wadhamini wengine ambao ni EACOP, TASAF, EWURA, PASS Trust, NIC, BRELA, National Construction Council, PPRA, TTCL, CBM, SELF MICROFINANCE, AGAKHAN FOUNDATION, TAWLA (MRADI WA MWANAMKE IMARA), TACAIDS, UTT AMIS, Benki ya ABSA, Benki ya AZANIA, Benki ya Maendeleo ya kilimo (TADB), eGA pamoja na Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Tanzania (TAA). Tunategemea kuendelea kushirikiana nanyi katika kutekeleza mipango mbalimbali inayolenga kuwawezesha watanzania.

Baada ya kusema hayo nawakaribisha sana kwenye kongamano la leo.

**NA ASANTENI SANA KWA KUNISIKILIZA**